

Standard 7 End Term 1 Exam, 2016

Soma kifungu kifuatavyo. Kinā nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu mianne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale ulivopewa.

Naam, wasemao husema kuwa elimu ni _____ 1 _____ gizani hung'aa, hakika waligonga _____ 2 _____ kwa kunena mambo ya ukweli kwani elimu kokote huangaza na kumeremeta kwa mmeto _____ 3 _____ _____ 4 _____ angani. Bila elimu mja _____ 5 _____ mkamilifu, wapo matajiri _____ 6 _____ lakini bado wana dosari _____ 7 _____ ni kukosa elimu. Elimu ni kiini _____ 8 _____ kila amali duniani, sera mbalimbali hutegemea elimu kwa hali na _____ 9 _____. Elimu ni _____ 10 _____ mjarabu ya maisha. Hewaa! Elimu ni maisha _____ 11 _____ vitabu. _____ 12 _____ _____ 13 _____ haina mwisho wala _____ 14 _____ hadi mtu atakapozikwa kaburini ndipo kwake elimu hukatika. Elimu haina mwisho _____ 15 _____ haitekeki.

- | | | | |
|----------------|--------------|----------------|----------------|
| 1. A. kurunzi | B. tochi | C. taa | D. mwangaza |
| 2. A. mwamba | B. ndipo | C. ukuta | D. vichwa |
| 3. A. ya | B. za | C. wa | D. mwa |
| 4. A. sahani | B. nyota | C. mwezi | D. jua |
| 5. A. hauwi | B. huwi | C. hawiwi | D. hawi |
| 6. A. pomoni | B. hohe hahe | C. tipwa tipwa | D. njori njori |
| 7. A. nalo | B. nayo | C. nao | D. nazo |
| 8. A. cha | B. ya | C. vya | D. za |
| 9. A. staha | B. rangi | C. mali | D. taadhma |
| 10. A. daawa | B. dawa | C. chanzo | D. njia |
| 11. A. na | B. si | C. ni | D. haina |
| 12. A. Michezo | B. Elimu | C. Utoto | D. Maisha |
| 13. A. huyo | B. huyu | C. hii | D. hiki |
| 14. A. awali | B. alfa | C. mwanzo | D. kilele |
| 15. A. lakini | B. ili | C. ila | D. wala |

Kutoka swali la 16-30 chagua jibu sahihi

16. Kitenzi lina katika kauli ya kutendewa ni _____.
A. liza B. lilishwa
C. liliwa D. lilia
17. Unapoambiwa "**tuonane kesho**" jibu lako litakuwa _____.
A. asante B. pia nawe
C. majaliwa D. kwako pia
18. **Kanusha:**
Asingekuja asingenipata
A. Asingelikuja asingalinipata
B. Hangekuja hangenipata
C. Angekuja angenipata
D. Hakuja wala hakunipata
19. Jimbi ni kwa koo kama vile mjomba ni kwa _____.
A. shangazi B. halati
C. ami D. wif
20. Shilingi ilipoanguka sakafuni ilitoa sauti gani?
A. Tiri! B. Tang'!
C. Kiii! D. Kacha!
21. Sifa kutokana na kitenzi angaza ni _____.
A. mwangazi B. mwanya
C. milki D. angavu
22. $\frac{3}{9}$ kwa maneno ni _____.
A. tusui B. tatu kwa tisa
C. thuluthi tisa D. tusui tatu
23. Ni pambo lipi huvalia shingoni?
A. Hina B. Kidani
C. Kibanio D. Kipuli

24. **Tambua kiyunishi katika sentensi:**
Watoto wengi walikimbia sana.
A. watoto B. wengi
C. sana D. walikimbia
25. **Chagua sentensi ilivoakifishwa vyema**
A. Kimani (aliyefungia timu yao bao) ni yule mfupi
B. Mwalimu alisema, njooni mnisadie
C. Ana, hao ni upuzi
D. Mnataka kuchapwa
26. **Tena sentensi venye 'O' rejeshi tamati**
A. Mtu anayetembea ni waziri
B. Maembe yatakayoliwa ni yale yameiva
C. Popote utakapoenda utampata
D. Mtu aendeshaye meli huitwa nahodha
27. _____ umeandaliwa na mpishi _____.
A. Mjusi, mphuzi B. Mdunzi, mjusi
C. Mchuzi, mjuzi D. Mjuzi, mjuzi
28. Kisawe cha barobaro ni _____.
A. kijana B. mvulana
C. gashi D. mwanamwali
29. Milima mingi ikiwa pamoja huitwa _____.
A. safu B. korija
C. numbi D. milima
30. Andika udogo wa **ndovu**
A. kijindovu B. jindovu
C. kidovu D. kandovu

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40

Kwa miaka mingi wanaume wamekuwa wakishiriki ulevi wa pombe **mchana kutwa**. Inasemekana wao husahau majukumu yao ya kijamii. Kauli hii ina ukweli fulani ndani yake.

Siku hizi swala la ulevi linaelekea **kuchakua mwelekeo mpya**. Wanawake wengi siku hizi wameufuata mkondo wa ulevi. Uchunguzi unaonyesha kuwa idadi ya wanawake wanaokunywa pombe inaendelea kuongezeka kila uchao.

Katika vilabu vya mjini kukutana na wanawake wenye pete vidoleni, wakimimina vile usiku kucha si ajabu. Ajabu zaidi ni kwamba wake hawa hawaandamani na waume wao. Hulewa peke yao na kukesha vilabuni hivyo. Wasichana wenye umri wa kadri pia wanajitoma katika vilabu hivi bila kuona haya.

Baadhi ya wataalamu wanasema kuwa wanawake hujitosa ulavini ili kujaribu kuepuka matatizo yanayoshirikiana na ndoa. Wengine hulewa ili kupunguza uzito wa miili yao. Aidha, uteza, u josefu wa kazi, dhuluma na ushawishi wa marafiki zimetajwa kama sababu arhazo zinawapelekea wanawake kulewa.

Kulingana na sayansi, pombe haina faida yoyote ya kiafya katika mwili wa binadamu. Mtu hunywa pombe kwa kiburudisho nafsi zao tu. Wanawake wanapolewa sana hushindwa kujidhibiti kama wanaume. Ni rahisi sana kwa mwanamke akilewa.

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50

Katika kijiji cha Mwaragania waliishi vijana wawili. Vijana hawa walikuwa masahibu wa kufa kuzitana. Hawakuachana. walitembea pamoja na kwenda shuleni pamoja. Hakika walikuwa uta na upote.

Ijapokuwa umri wa Hilda ulikuwa tofauti na wa Imani, jambo hili halikuutatiza urafiki wao Hilda alikuwa na umri wa miaka kumi na mitano na Imani alikuwa na miaka kumi na minane. Siku moja Hilda aliamshwa na Imani na kumwambia kuwa walifaa kuwa na pesa zao wenyewe.

Pesa hizo zingewasaidia kununua biskuti na vitu vingine vinavyopendwa na watoto. Mwanzoni Hilda alikataa. Baada ya maneno machache alishawishika. Imani alionya kwamba Hilda asimwombe vitu vyake.

Pesa zenyewe zingepatikana kwa uchopezi. Katika wakati huo vijana hawa wakaanza kuwa wezi wa kuchopoa mifuko.

Siku za mwizi ni arubaini, wote wawili walitiwa mbaroni walipokuwa wakinyemelea mifuko ya watu waibe. Walipelekwa katika shule ya kurekembisha tabia. Hilda alijuta sana lakini majuto ni mjukuu huja baadaye.

- | | |
|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| 41. Hilda na Imani hawakuwa _____
A. marafiki wakubwa
B. wametoka katika mji wa Mwaragania
C. wanafunzi
D. wavulana | 46. Hama ya vijana hawa kupata pesa ilikuwa _____
A. kutimiliza haja ya kukidhi mahitaji ya kimsingi
B. kununua vipochopocho vinavyopendwa na watoto
C. kukimu maisha yao
D. kulipa karo |
| 42. Marafiki wa kufa kuzikana ni _____
A. marafiki wenye tabia mbaya
B. ambao wangependena hata wakifa
C. marafiki wakubwa
D. marafiki wanaochukiana | 47. Vijana hawa walikubaliana _____
A. kufanya makosa ya jinai
B. kufanya wizi wa kimabavu
C. kununua peremende na biskuti
D. kufanya wizi wa mifukoni |
| 43. Tofauti ya umri wa Hilda na Imani nikuwa ni _____
A. mitano
B. thelathini na mitano
C. miaka mitatu
D. miezi sitini | 48. Hilda alijuta kwa sababu _____
A. Imani alikuwa rafiki yake
B. Alichapwa alipatiwa mbaroni
C. Alisikiliza mawaidha mabaya ya Imani
D. Hawakugawanya pesa kwa usawa |
| 44. Ni jambo gani halikuweza kutatiza urafiki wao?
A. Tofauti ya miaka
B. Pesa zao
C. Majina yao
D. Kazi zao | 49. Kwa kawaida mwizi ashikwapo _____
A. hufungwa jela moja kwa moja
B. huhukumiwa na polisi
C. huadhibiwa na kusamehewa
D. hufikishwa kortini |
| 45. Maana ya "kutiwa mbaroni" ni _____
A. kufungwa kortini
B. kushikwa na polisi
C. kupelekwa kortini
D. kushikwa kwa nguvu | 50. Kichwa mwafaka ni _____
A. watoto wezi
B. kikulacho ki nguoni mwako
C. Nazi mbovu harabu ya nzima
D. Baniani mbaya kiatu chake dawa |